

# UFUGAJI BORA WENYE KUPUNGUZA UMASKINI, MIGOGORO NA KULETA TIJA

## Utangulizi

- Karibu 14% ya ng'ombe wa asili nchini wanafugwa katika mfumo wa kuhamahama
- 80% katika mfumo wa Kilimo-Ufugaji
- Ng'ombe wa Asili huchangia > 90% ya nyama inayozalishwa nchini
- > 70% ya maziwa yanayozalishwa nchini
- Uwezo wa kuzaliana kwa mwaka ni 40 - 50%

- ❑ Vifo vya ndama ni wastani wa 30-40% kwa mwaka
- ❑ Muda wa mzao mmoja hadi mwingine ni > ya miezi 18
- ❑ Uzito wa kuchinjwa ni kilo 250-300 katika umri wa miaka 6-7
- ❑ Kiwango cha ngombe wanaouzwa kwa mwaka ni 8 - 10%
- ❑ Nyanda za Malisho huendelea kudidimia (Umiliki wa Jumuiya)
- ❑ Migogoro isiyoisha baina ya Wafugaji na Wakulima wa Mazao
- ❑ Idadi ya watu inazidi kuongezeka

# NINI KIFANYIKE ILI KUBORESHA UZALISHAJI?

- ❑ Wafugaji waache kuhamahama
- ❑ Wafugaji wamiliki ardhi na kuwekeza katika miundombinu ya ufugaji bora
- ❑ Uzalishaji ulenge soko la nje na la ndani
- ❑ Inapendekezwa teknolojia ya Uanzishwaji wa ranchi ndogondogo/Kati utumike ili kuleta mageuzi katika uzalishaji wa ngombe wa Asili kwa ajili ya kuzalisha nyama na maziwa nchini.

# MAHITAJI YA UANZISHWAJI WA RANCHI NDOGONDOGO

- Wafugaji/Wadau wahamasishwe kumiliki ardhi rasmi ili kuwekeza katika ujenzi wa miundo mbinu ya ufugaji bora kwa matumizi ya muda mrefu kulinda raslimali
- Upimaji wa ardhi na kuchukua sampuli za udongo katika eneo litakalotumika kwa matumizi ya ranchi
- Ujenzi wa padoki, vibanio, eneo la kulishia chakula cha nyongeza, kwa kuzingatia idadi ya ng'ombe au ukubwa wa ardhi iliyomilikiwa
- Wafugaji kujengewa uwezo juu ya matumizi ya teknolojia ya ranchi ndogo ndogo au za Kati

❑ Uanzishwaji wa malisho katika padoki zilizotengenezwa kwa kutumia aina bora za malisho kwa kila eneo husika

❑ Uvunaji wa maji kwa kutumia mbinu mbalimbali mfano maji ya mvua, kuchimba visima kwa matumizi ya mifugo na binadamu

❑ Uboreshaji wa afya ya mifugo kwa kuzingatia njia bora za kudhibiti magonjwa (tiba, chanjo na uogeshaji)

## Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi



Matumizi ya ranchi ndogondogo ili kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama

## Halmashauri ya wilaya ya Mbozi



Uandaaji wa mbegu za malisho bora

## Halmashauri ya Wilaya ya Mulele - Mpanda



Uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho aina ya *Rhodes*